

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

687

VITENDO VYA KUJIFUNZA HAIBA NA MICHEZO

Mwaka: 2022

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma maelekezo **yote** yaliyopo katika kijitabu chako cha kujibia.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha **mtihani**.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Kuna michezo ambayo huhitaji watoto zaidi ya mmoja kushirikiana ili kufikia lengo, kwa mfano mchezo wa rede. Eleza kwa kifupi faida nne za watoto kushirikiana katika michezo.
2. Fikiria umealikwa na Afisa Elimu Kata kutoa semina ya utengenezaji wa vifaa vya michezo vya watoto wa Elimu ya Awali. Eleza kwa kifupi hatua nne za utengenezaji wa vifaa utakazoziwasilisha kwa walimu wenzako.
3. Watoto wa Elimu ya Awali hujifunza zaidi kwa kutumia vifaa na vitendo kuliko nadharia katika mazingira ya kucheza. Kwa kutumia dondoo nne, kubaliana na kauli hii.
4. Ukiwa kama mwalimu wa Somo la Vitendo vya Kujifunza Haiba na Michezo, bainisha michezo minne inayoweza kutumika katika kuimarisha afya ya viungo mbalimbali katika miili ya watoto wa Elimu ya Awali.
5. Matumizi ya mbinu anuai katika ufundishaji huwafanya wanafunzi wahamasike muda wote wa kipindi na wajifunze kwa furaha na kujenga nidhamu. Eleza kwa kifupi mbinu nne unazoweza kutumia katika kufundisha nidhamu kwa watoto wa Elimu ya Awali.
6. Wanafunzi wa Elimu ya Awali wana michezo mingi na hawawezi kutulia sehemu moja hata kwa dakika ishirini. Eleza kwa kifupi mbinu nne unazoweza kutumia kudumisha nidhamu katika michezo.
7. Ili maandalizi ya mchezo wowote ule yakamilike, vifaa vya kufundishia vinahitajika. Eleza kwa kifupi sifa nne za vifaa bora vya kufundishia na kujifunza michezo ya ndani.
8. Mwalimu wa Elimu ya Awali anashauriwa kuandaa azimio la kazi kabla ya muhula kuanza. Kwa kutumia hoja nne, eleza kwa kifupi umuhimu wa maandalizi hayo katika somo la Vitendo vya Haiba na Michezo.
9. Walimu wazoefu kazini hawaoni umuhimu wa kuandaa andalio la somo. Kwa kutumia hoja nne eleza kwa kifupi nini kitatokea iwapo mwalimu wa Elimu ya Awali hatatumia andalio la somo katika ufundishaji wake.
10. Moja kati ya maandalizi ya ufundishaji ambayo mwalimu anapaswa kufanya ni andalio la somo. Bainisha kwa kifupi vyanzo vinne ambavyo vitamsaidia mwalimu katika kuandaa andalio la somo la Vitendo vya Kujifunza Haiba na Michezo.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

11. Adhabu ya viboko imekuwa ikitumika sana katika kudhibiti nidhamu ya watoto wa Elimu ya Awali pindi wanapokosea. Kwa kutumia hoja tano jadili hasara zinazotokana na adhabu hiyo kuhusishwa katika ujifunzaji wao.
12. "Kumfundisha mtoto wa Elimu ya Awali Vitendo vya Haiba na Michezo ni kupoteza muda." Pinga kauli hii kwa kufafanua hoja tano.
13. "Mtoto mwenye tabia njema mara nyingi huwa na maendeleo mazuri kitaaluma." Thibitisha usemi huu kwa kutumia hoja tano.
14. Siku moja mwalimu Mkuu alimkuta mwalimu Haji akifundisha kwa kutumia michezo ya ndani. Kwa mtazamo wa Mwalimu Mkuu, hayo yalikuwa matumizi mabaya ya muda wa kujifunza. Tumia hoja tano kumwelimisha mwalimu Mkuu manufaa ya kitendo alichokifanya mwalimu Haji.